HOTUBA YA MHESHIMIWA SAMIA SULUHU HASSAN, MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KWENYE KILELE CHA MAADHIMISHO YA SIKU YA MAZINGIRA DUNIANI, YALIYOFANYIKA KITAIFA BUTIAMA, MKOANI MARA TAREHE 4 JUNI, 2017

Mhe. January Y. Makamba (Mb),
Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano na Mazingira;
Mhe. Dkt. Charles Mlingwa, Mkuu wa Mkoa wa Mara;
Mhe. Luhaga J. Mpina (Mb),
Naibu Waziri , Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano na Mazingira;
Profesa Faustin Kamuzora, Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais,
Mheshimiwa Mwenyekiti wa Mji wa Musoma;
Bw. A. Mapunda, Katibu Tawala wa Mkoa wa Mara,
Katibu wa CCM wa Mkoa wa Mara;
Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya;
Waheshimiwa Wabunge;
Waheshimiwa Madiwani;
Viongozi mbalimbali wa Vyama vya Siasa;
Viongozi wa Dini na Madhehebu mbalimbali;
Ndugu Wanahabari;
Wageni Waalikwa;
Ndugu Wananchi;
Mabibi na Mabwana.

Kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyenzi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia uzima na afya njema, na kutuwezesha kukusanyika

hapa Butiama siku ya leo ili kuhitimisha maadhimisho haya ya Siku ya Mazingira Duniani.

Nitumie fursa hii kuupongeza Mkoa wa Mara kwa kukubali kuwa Mwenyeji wa maadhimisho ya siku hii Kitaifa. Napenda kuushukuru uongozi wa Mkoa na wadau mbalimbali walioshiriki kwa njia moja au nyingine katika kufanikisha maadhimisho haya. Nimearifiwa kuwa tangu tarehe 1 Juni kumekuwepo na shughuli zinazohusu utoaji elimu kuhusu hifadhi ya mazingira katika maeneo mbalimbali mkoani Mara na pia nimepokea mipango ya maadhimisho kutoka mikoa yote nchini. Natumia fursa hii kupongeza viongozi na wananchi wa mikoa yote kwa kuadhimisha siku hii kwa vitendo. Hongereni sana! Kwa namna ya pekee napenda kuushukuru tena uongozi wa mkoa na wananchi wa Mara kwa mapokezi mazuri na ukarimu mliouonesha kwangu na kwa wageni wote waliofika hapa Mkoani. Asanteni sana na Mwenyezi Mungu awazidishie moyo huu wa ukarimu.

Ndugu Wananchi;

Leo Watanzania tunaungana na jamii ya Kimataifa Duniani kote kuadhimisha kilele cha Siku ya Mazingira Duniani. Siku hii muhimu huadhimishwa kwa lengo la kukumbushana wajibu wetu kama jamii na kuelimishana umuhimu wa kuhifadhi na kutunza mazingira kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo. Umati huu ni kielelezo tosha cha kuonesha ni jinsi gani mnayapa umuhimu wa kipekee masuala ya hifadhi na usimamizi wa mazingira. Ninawapongeza na kuwashukuru kwamba pamoja na shughuli nyingi muhimu mlizonazo, mmeweza kutenga muda na kuhudhuria kwenye kilele cha Siku ya Mazingira Duniani. Kwa kawaida siku ya kilele huwa ni tarehe 5 Juni lakini mwaka huu tumeamua kufanya leo ili

wananchi wengi waweze kushiriki na pia kuzingatia leo ni siku ya Jumapili ambapo wananchi wengi wanapumzika.

Ndugu Wananchi;

Kaulimbiu ya Siku ya Mazingira Duniani mwaka huu ni **“ Mahusiano Endelevu Kati ya Binadamu na Mazingira” kwa lugha ya kiingereza ni *Connecting People to Nature*.** Kaulimbiu hii inatuhimiza jamii yote kuhifadhi Mazingira kwa kuzingatia uhusiano wa kutegemeana uliopo kati ya maisha ya binadamu na maliasili hususan, katika shughuli zetu za kijamii na kiuchumi na Mazingira. Kwa kuhifadhi mazingira tutakuwa tunajihakikishia kuwa dunia hii itakuwa salama na itatupatia mahitaji yetu kwa wakati huu na hata baadaye. Mfumo wa kutegemeana kati yetu binadamu, viumbe wengine na mazingira ni muhimu katika kutuhakikishia maisha bora na salama kwa kizazi chetu na vizazi vijavyo. Kutozingatia hifadhi ya mazingira kunaweza kusababisha kuparanganyika kwa mfumo huu na kufanya maisha yetu nay a wajao kuwa kwenye mashaka makubwa.

Ndugu Wananchi;

Pamoja na kuwa na Kaulimbiu ya kimataifa, hapa nchini tunao utaratibu wa kuwa na Kaulimbiu yetu inayoongoza maadhimisho haya kulingana na vipaumbele vyetu Kitaifa. Hivyo, Kaulimbiu ya kitaifa kwa mwaka huu ni “ **Hifadhi ya Mazingira: Muhimili kwa Tanzania ya Viwanda” .** Kaulimbiu hii inatuhimiza jamii ya watanzania kuwa, wakati tukielekea kwenye uchumi wa kipato cha kati kupitia viwanda, ni muhimu kwa kila mmoja wetu kuzingatia hifadhi ya mazingira. Tunaamini kuwa viwanda ni moja ya njia ya kutupeleka katika uchumi wa kati kwa haraka na

kupunguza umasikini miongoni mwa jamii na kwamba hali hiyo itafikiwa iwapo tutazingatia sheria na kanuni za maendeleo endelevu.

Ikumbukwe kuwa ili kuwa na Tanzania ya viwanda endelevu hatuna budi kuhakikisha kuwa viwanda vyetu vinatumia maliasili chache katika uzalishaji na kuzalisha taka chache iwezekanavyo ili kudhibiti uchafunzi wa mazingira bila kuathiri malengo ya uzalishaji wa bidhaa tarajiwa.

Ndugu Wananchi;

Ni ukweli usiopingika pia kuwa kuanzisha au kufufua viwanda kunahitaji umakini na uzingatiaji wa masuala ya mazingira ili kuhakikisha kuwa viwanda hivi vinaleta tija na haviathiri mazingira na maisha ya viumbe vingine tukiwemo sisi wanadamu. Sheria ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 na kanuni zake zimewekwa ili kuhakikisha kuwa uwekezaji wowote ule unaofanyika unazingatia hifadhi ya mazingira. Vilevile, Tathmini ya Athari kwa Mazingria (TAM) ndiyo njia iliyopo kisheria itakayotuhakikishia usalama wa mazingira na uchumi endelevu kutokana na uzalishaji viwandani. Muhimu ni kuhakikisha kuwa utaratibu unafuatwa katika hatua za kusanifu, kujenga, kuendesha na uzalishaji viwandani ili kuepuka madhara na uchumi usiokuwa endelevu nchini.

Zipo faida nyingi za kuhifadhi na kusimamia mazingira zitakazotokana na Tanzania kuwa na viwanda vingi. Ukiacha kwamba ajira itapatikana kwa wingi, kuwepo kwa viwanda pia kutatupeleka kwenye uchumi wa kati na hivyo wananchi wengi kuondokana na umaskini na kutuepusha shughuli za uharibifu wa mazingira utokanao na utegemezi kwenye mifumo-ikilojia.

Ndugu Wananchi;

Kama nilivyosema awali, kitaifa, maadhimisho haya yanafanyika hapa Butiama, Mkoani Mara ambapo Watanzania kote nchini, Mikoa, Wilaya na Vijiji wanaungana kwa pamoja kuadhimisha siku hii kwa lengo la kuelimishana na kuhamasishana kuhusu umuhimu wa kutunza na kuhifadhi mazingira. Aidha, maadhimisho haya yanaendelea kote duniani na Kimataifa, maadhimisho haya yanafanyika nchini Canada. Lengo kubwa la kuadhimisha Siku ya Mazingira Duniani kitaifa hapa Butiama, ni kumuenzi Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere kwa juhudi na utashi wake wa kuhakikisha rasilimali za nchi hii zinatumika na zinaendelea kuwepo kizazi hadi kizazi. Haya aliyaeleza katika maandiko yake mengi ikiwemo Ilani ya Arusha ya mwaka 1961. Aidha, Baba wa Taifa hakuishia kuyasema tu bali aliyaishi na aliyatekeleza maneno yake kwa vitendo. Ndiyo maana leo tunashuhudia kuwepo kwa msitu wake aliousimamia na kuhakikisha anauendeleza wakati wa uhai wake. Hivyo, sisi sote tuige mfano wake kwa kuhakikisha tunaacha alama na kumbukumbu za kuonesha wakati wa uhai wetu tulikuwa na mahusiano endelevu kati yetu na mazingira.

Ndugu Wananchi;

Tunapoadhimisha Siku ya Mazingira Duniani, tunapaswa tuchukue hatua za kuelimishana na kuhamasishana ili kila mmoja wetu ashiriki katika juhudi za kuwa na uchumi unaozingatia hifadhi ya mazingira. Juhudi na ushiriki wa kila mmoja wetu, wawekezaji, wafanyakazi na wadau wote katika harakati hizi za kuwa na viwanda na hatimaye kufika kwenye uchumi wa kati, ndiyo nguzo kuu ya mafanikio katika kufanikisha azma ya Serikali ya kuwa nchi ya uchumi wa kati.

Maadhimisho haya tuyatumie kukuza uelewa kwa jamii, kuchochea na kuongeza utashi wa kisiasa katika masuala ya hifadhi na usimamizi wa

mazingira. Nitumie fursa hii kuipongeza Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kuruhusu wananchi kutembelea mbuga zetu na hifadhi za taifa bila kiingilio kuanzia tarehe 2 hadi 4 Juni 2017. Fanyeni hivi kila mara angalau mara moja kila mwaka. Utaratibu huu umekuwa ni moja ya kichocheo cha kuhamasisha wananchi ili wawe na mahusiano rafiki na mazingira, hii ni kwa sababu ya ukweli kwamba, unapoona ndipo unaelewa na kuamini (seeing *is believing*). Hivyo basi tuchukulie maadhimisho haya kuwa ni fursa kwetu ya kutafakari kuhusu mchango wa kila sekta na kila mmoja wetu na changamoto zinazoweza kujitokeza na hivyo kuweka mikakati muafaka ya kuipeleka nchi kwenye uchumi wa kati.

Ndugu Wanachi;

Katika kuadhimisha Siku ya Mazingira Duniani nimeshuhudia baadhi ya shughuli zilizofanywa wakati wa maadhimisho haya hapa mkoani Mara hususan, Wilayani Butiama. Shughuli nilizozishuhudia hapa Butiama ni pamoja na:

- Kupanda miti na kutangaza hatua za kuuhifadhi na kuulinda msitu ambao Baba wa Taifa aliuhifadhi;
- Kuendesha mijadala kuhusu masuala mabalimbali yanayohusu maisha ya Watanzania, shughuli wanazofanya na hifadhi ya mazingira;
- Kuendesha Kongamano la viongozi kuhusu mchango wa Mwalimu Nyerere kwenye hifadhi ya mazingira nchini na umuhimu wa mazingira kwa mustakabali wa nchi yetu na masuala ya msingi ambayo Baba wa Taifa aliyasisitiza; na
- Maonesho ya shughuli mbalimbali za hifadhi ya mazingira.

Hizi ni shughuli chache tu kati ya nyingi zilizotekelezwa mkoani Mara wakati huu wa maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani.

Ndugu Wananchi;

Jukumu letu la msingi ni kuyatafutia ufumbuzi matatizo yanayohusu uzingatiaji hifadhi na usimamizi wa mazingira tunapofanya shughuli za kujiletea maendeleo.. Yako mambo mengi ambayo yanahitaji mikakati ya kudumu ili kuhakikisha kwamba shughuli za maendeleo ya kiuchumi haziathiri mazingira. Njia mojawapo ya kutufanya tuzingatie masuala ya mazingira katika mchakato wa maendeleo ni kukumbushana na kueleimishana. Hii ndiyo sababu katika maadhimisho ya mwaka huu kumekuwepo na utaratibu wa kufanya majadiliano ya mada mbalimbali kuhusu hifadhi ya mazingira.

Lengo la kuendesha na kufanya kongamano na mijadala hii ni kuelimisha na kuhamasisha wananchi wote juu ya utunzaji na hifadhi ya mazingira.

Ndugu Wananchi;

Kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, nitoe wito kwa watendaji wote na watanzania wote kwa ujumla kufanya yafuatayo:

a) kuhakikisha tunaongoa mifumo ikolojia ili tuwe na maji ya kutosha na kuhifadhi bioanuai;
b) kupanda aina ya miti inayofaa katika maeneo husika na kuitunza;
c) kuhifadhi misitu na uoto wa asili;
d) kuepuka uchomaji moto ovyo wa misitu na uoto wa asili;
e) Kuacha ukataji miti kiholela;
f) kudhibiti uchafuzi wa mazingira utokanao na shughuli za viwanda; na
g) kudhibiti uchimbaji wa madini na kilimo kisicho endelevu.

Hivyo, watendaji wote muhakikishe kwamba mnasimamia kikamilifu masuala ya hifadhi na usimamizi wa mazingira, mkizingatia kwamba dhambi ya kuharibu mazingira haisameheki. Na sisi wananchi tuwe wasikivu na tutekeleze maelekezo tunayopewa na viongozi au wataalamu wetu yenye mstakabali wa taifa letu.

Kwa kumalizia napenda, kuushukuru tena na kuupongeza Uongozi wa Mkoa wa Mara kwa maandalizi mazuri ya Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani ya mwaka 2017. Aidha, nazipongeza Halmashauri, Taasisi, Kampuni, Vikundi na Watu binafsi kwa ushirikiano wao katika kufanikisha maadhimisho haya~~.~~ kwa kutoa muda, fedha, nguvukazi, utaalamu na ushauri. Shukurani zangu hazitakuwa kamili iwapo sitapongeza sana wazo la Viongozi na Watendaji wa Ofisi yangu chini ya uongozi makini wa Waziri wa Nchi, Mheshimiwa January Makamba(Mb.) kupendekeza Shughuli hii ifanyikie hapa Butiama. Ninawashukuru sana kwa maandalizi na kwa kutuwezesha kuadhimisha siku za Mazingira Duniani pamoja na kumuenzi Baba wa Taifa kwa kuunga mkono harakati zake za kuhifadhi mazingira.

Mwisho kabisa nasisitiza, Tuwe **na Mahusiano Endelevu Kati yetu sisi Binadamu na Mazingira.** Baada ya kusema haya natamka kwamba, Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani Kitaifa hapa Butiama Mkoani Mara yamefikia kilele.

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza.